



**Chama cha Ukuzaji wa Kiswahili Duniani**

**Global Association for the Promotion of Swahili**

**CHAUKIDU**

---

**Kongamano la Kimataifa la Tano la CHAUKIDU KAMPALA, Uganda**

**MADA KUU:** *Ukuaji wa Kiswahili Duniani na Ustawi wa Lugha Nyingine za Kiafrika*

**MAHALI:** Kampala– Chuo Kikuu cha Kyambogo, Kampala Uganda

**TAREHE:** Desemba 13- 15, 2019 (Jumamosi & Jumapili)

**Warsha:** Desemba 13, 2019 (Ijumaa)

**Mada:** Uzoefu na Mbinu za Ufundishaji wa Kiswahili

Kuwasili – Alhamisi Desemba 12, 2019

**WASHIRIKI / WALENGWA:** Wadau wote wa Kiswahili duniani kote

---

Hoja ya kwamba Kiswahili ni mojawapo ya lugha za mawasiliano mapana (*lingua francas*) katika ukanda wa Afrika ya Mashariki na Kati, ni suala ambalo halihitaji mjadala. Hata hivyo, kwamba *lingua francas* huambatana na faida na hasara au huwa na athari chanya na hasi katika jamii husika, ni madai ambayo yameibua mjadala mkali ndani na nje ya wigo wa kiakademia duniani kote. Mjadala huu uko hai, unaendelea na unataka majibu.

Mintaarafu mjadala huu, Kongamano la tano la kimataifa la CHAUKIDU linalenga kutoa fursa ya kuvinjari na kutafakari kwa kina kuhusu uhusiano uliopo kati ya ukuaji wa Kiswahili na ustawi au uviaji (udumazaji) wa lugha nyingine za Kiafrika katika ukanda wa Afrika ya mashariki. Kwa kufanya hivi, Kongamano hili litakuwa limetoa mchango mkubwa katika mjadala mpana ambao hatimaye matokeo yake yanaweza kuwa na manufaa ya kitaaluma, kisera, kijamii, na hata kintazamo katika maisha ya kila siku ya wanajamii wa Afrika ya Mashariki. na kwingineko duniani.

Sambamba na lengo hilo hapo juu, Kongamano la tano la kimataifa la CHAUKIDU litakalofanyika jijini Kampala, nchini Uganda linalenga kuwaleta pamoja wadau mbalimbali wa Kiswahili duniani kote ili kujadili uendelezaji na unawirishaji wa Kiswahili na lugha nyingine za Afrika Mashariki. Ni matarajio yetu kuwa wadau wengi wa Kiswahili watachangamkia fursa ya kujadili na kuchangia masuala haya kupitia mawasilisho, na mazungumzo na pia ni matumaini yetu kuwa mijadala hii itachochea uendelezaji wa lugha yetu adhimu ya Kiswahili pamoja na lugha zetu nyingi zinazozungumzwa katika eneo la Afrika ya Mashariki na Kati.

Kwa kuhitimisha, Kongamano hilo litawapa fursa wapenzi na wakereketwa wa Kiswahili, walimu, wanafunzi, watafiti, waandishi, wanahabari, wanasiasa, wasanii, wakuzaji wa mitaala, maafisa wa lugha, wachapishaji, wanasayansi, wafanyabiashara, n.k., kubadilishana na kuelimishana kuhusu maarifa, weledi, tajiriba, taaluma n.k. zinazohusiana na lugha ya Kiswahili.

## **MADA NDOGO/MAJOPO**

Kiswahili na siasa/utawala/uongozi (usalama, ulinzi, uhamiaji, diplomasia, nk)

Kiswahili na utamaduni (jadi, imani za kidini, michezo, ujenzi, mavazi, vyakula, mapishi, nk) Kiswahili na uchumi (biashara, viwanda, kilimo, ufugaji, uvuvi, utalii, madini, miundombinu) Kiswahili na elimu (ngazi za elimu, lugha ya kufundishia/kujifunzia, taaluma, tafiti, uchapishaji)

Kiswahili na Sanaa (muziki, maigizo/filamu, vibonzo, nk)

Kiswahili na fasihi (nadharia, simulizi, andishi, riwaya, ushairi, tamthiliya, nk)

Kiswahili na isimu (maumbo, miundo, nadharia, nk)

Kiswahili na lugha za Kiafrika (kujengana, kukamilishana, nk)

Kiswahili na upashaji habari (magazeti, vijarida, redio, runinga, mitandao ya kijamii, blogu, nk) Kiswahili kwa wageni (Afrika, Ulaya, Asia, Amerika, nk)

Kiswahili na lahaja zake (Kiswahili cha mitaani, kiSheng, kiSwanglish, nk.) Kiswahili na teknolojia na utandawazi

Kiswahili na uhamasishaji, uenezi (maarifa, itikadi, teknolojia, nk)

Kiswahili na vyama vya ushirika na maendeleo yake

Utafiti wa Kiswahili na taaluma zake

---

Tarehe ya mwisho kupokea ikisiri: tarehe 31 Mei, 2019

Tafadhalini tumeni ikisiri zenu kabla ya tarehe ya makataa kwa:

chaukidu2019UG@gmail.com

Tangazo la ikisiri zilizokubaliwa: tarehe 15 Julai, 2019

Tarehe ya makataa ya miswada kamili ya makala: tarehe 30 Septemba 2019

**Ada za kushiriki:**

1. Washiriki kutoka Afrika Mashariki: \$40.00
2. Washiriki kutoka sehemu nyingine Afrika: \$50.00
3. Wanafunzi wote : \$20.00
4. Washiriki kutoka nje ya Afrika: \$150.00

Jisajili mapema kabla ya tarehe 30 Septemba 2019 na huenda ukaokoa kiasi fulani cha ada!